JARIDA LA RS RUVUMA

TOLEO LA OKTOBA,2026

RUVUMA YETU

Na.0004 Tembelea ;www.ruvuma.go.com RUVUMA IVUME KWA MAENDELEO

RUVUMA YAFIKIA ASILIMIA 64.5 YA LENGO LA USAJILI WA BIMA YA AFYA KWA WOTE



Mkoa wa Ruvuma umefanikiwa kusajili kaya 7,278 kati ya kaya 11,282 zilizokuwa zimelengwa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, sawa na asilimia 64.5. Aidha, wanufaika 19,001 walisajiliwa kati ya walengwa 50,532, sawa na asilimia 37.6.

Akizindua awamu ya pili ya usajili wa Bima ya Afya kwa Wote leo Oktoba 22, 2026 mkoani Ruvuma, Mkuu wa Mkoa huo, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas, amesema Serikali inaendelea kusisitiza umuhimu wa wananchi kujiunga na mfumo wa bima ya afya ili kuhakikisha wanapata huduma za matibabu kwa uhakika na kwa gharama nafuu.

Amesema kuwekeza katika bima ya afya ni kuwekeza katika ustawi wa wananchi, kwani gharama za matibabu zinazoweza kujitokeza ghafla huwa mzigo mkubwa kwa familia nyingi, huku bima ikitoa kinga dhidi ya changamoto hizo za kifedha.

Pamoja na mambo mengine, amewaagiza viongozi wa mkoa na wilaya kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kujiunga na bima hiyo, kuweka malengo mahsusi ya uandikishaji na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mpango huo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Mhe. Kisare Makori, amesema mafanikio ya utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote yanategemea ushirikiano wa karibu kati ya viongozi, wataalamu wa afya na wananchi, huku akiahidi kuendeleza ushirikiano huo ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Wakili Mary Gasper Makondo, amesema mkoa umejipanga kikamilifu kuhakikisha awamu ya pili ya usajili inafanikiwa na kuwafikia wananchi hadi ngazi ya chini kabisa, huku akiwapongeza watumishi wa afya na viongozi mbalimbali kwa mchango wao katika utekelezaji wa huduma hiyo.

Kwa upande mwingine, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Dkt. Louis Chomboko, amesema awamu ya kwanza ilikumbwa na changamoto za kiufundi na kiteknolojia, ikiwemo kuchelewa kwa taarifa za usajili, lakini mifumo hiyo sasa imeboreshwa ili kurahisisha ukusanyaji wa takwimu na usajili wa wananchi.





MLEZI WA CCM RUVUMA ASISITIZA UMOJA NA MSHIKAMANO



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mlezi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Ruvuma, (MCC), Hamad Hassan Chande amewataka viongozi na wanachama wa chama hicho kuendeleza umoja, mshikamano na ushirikiano katika kukijenga na kukiimarisha chama ili kuendelea kuwapatia maendeleo wananchi.

Chande amesema hayo leo Novemba 2, 2026, mara baada ya kuwasili na kuzungunza na viongozi na wanachama wa chama hicho licha ya kupongeza uongozi wa Mkoa huo kwa jitihada kubwa za kuendelea kukijenga chama kwa lengo la kulipatia Taifa maendeleo.

"Nimekuja kuungana nanyi ndugu zangu kwa lengo moja tu, nimekuja kuimarisha Chama Cha Mapinduzi, ujenzi wa Chama Cha Mapinduzi, kipo imara, kipo fiti, lakini lazima tukae pamoja ili tujenge kwa pamoja" Chande

Katika hatua nyingine, Chande amemshukuru Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Taifa, kwa kumuamini kuwa mjumbe na kuwatumikia wanachama na wananchi wa Mkoa huo, huku aliweka dhamira ya dhati katika kuimarisha chama kikamilifu kwa kushirikiana na uongozi na wanachama wa Mkoa huo.





RC RUVUMA AITAKA NAESA KUSOGEZA HUDUMA ZA UGANI KARIBU NA WAKULIMA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, ameitaka Wakala wa Taifa wa Huduma za Ugani (NAESA) kuhakikisha huduma za ugani zinawafikia wakulima kwa karibu kupitia uwepo wa ofisi katika ngazi za halmashauri na utekelezaji wa majukumu yake kuanzia ngazi ya kata, ili kuongeza tija katika uzalishaji, kuwaunganisha wakulima na masoko na kuinua kipato chao.

RC Abbas ametoa wito huo wakati akipokea wataalamu na maafisa wa NAESA waliofika waliofika kujitambulisha katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa lengo la kutoa elimu kuhusu majukumu ya wakala huo, maana ya huduma za ugani, namna utakavyotekeleza shughuli zake mkoani humo pamoja na mikakati ya kusogeza huduma hizo karibu na wakulima kupitia ofisi za halmashauri.

Ahmed amesema Mkoa wa Ruvuma una fursa nyingi za kilimo ambazo zinahitaji kutumiwa ipasavyo, akieleza kuwa uwepo wa NAESA unapaswa kuwa chachu ya kuwasaidia wakulima kupata utaalamu na ushauri utakaowawezesha kuongeza uzalishaji na kunufaika zaidi na shughuli za kilimo.

Amesisitiza kuwa ni muhimu wakala huo kuhakikisha wataalamu wa ugani wanatekeleza majukumu yao kwa vitendo na kuwafikia wakulima katika maeneo yao, badala ya huduma hizo kubaki katika ngazi za juu za kiutawala, ili wakulima waweze kupata ufumbuzi wa changamoto zinazokabili shughuli zao za uzalishaji.

Kwa upande wake, Afisa Kilimo wa NAESA Makao Makuu Dodoma, Emmanuel Lucas Mtenga, amesema wakala huo umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha huduma za ugani nchini kwa kuwapatia wakulima elimu,



mafunzo na ushauri wa kitaalamu utakaowasaidia kuboresha mbinu za kilimo na kuongeza tija katika uzalishaji.

Mtenga amesema kupitia utekelezaji wa majukumu ya NAESA, wakulima wanatarajiwa kunufaika na huduma bora za ugani zitakazochangia kuongeza uzalishaji na kuboresha maisha yao. Aidha, Ahmed ameipongeza Wizara ya Kilimo kwa kuanzisha wakala huo na kumshukuru Rais kwa juhudi za kuimarisha sekta ya kilimo nchini.



SONGEA YAFUNGUA LANGO JIPYA LA UCHUMI: ABIRIA WAPANDA KUTOKA 3,900 HADI ZAIDI YA 22,000



Uwanja wa Ndege wa Songea mkoani Ruvuma sasa unaonekana kuwa zaidi ya sehemu ya kupandia ndege unaweza kuwa kichocheo kipya cha biashara, uwekezaji na utalii Ruvuma.

Dastan Komba, Meneja wa ATCL Mkoa wa Ruvuma, anasema kwa sasa uwanja huo una safari za ratiba siku nne kwa wiki ambazo ni Jumatatu, Jumatano, Ijumaa na Jumapili.

Komba anasema mwaka 2024/25 uwanja huo ulihudumia abiria 19,260 kupitia miruko 397 na kwamba Katika kipindi kilichofuata, idadi ya abiria ilifikia 20,667 kupitia miruko 463, kabla ya kufikia abiria 22,419 na miruko 558 katika mwaka wa fedha 2025/26.

Mabadiliko hayo yana msingi wa miundombinu. Serikali imewekeza zaidi ya Shilingi bilioni 37 katika ukarabati na upanuzi wa uwanja, huku runway ikiongezwa hadi mita 1,860 kutoka mita 1,625 na apron kuboreshwa kuhudumia ndege kubwa zaidi.

Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa,akiwa ziarani Songea alisema Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya jengo kubwa la kudumu la abiria.

Hapa ndipo fursa ilipo: ndege zikiongezeka, biashara inaweza kuongezeka. Mizigo ya anga, hoteli, utalii, mikutano na uwekezaji vinaweza kuifanya Songea kuwa lango la uchumi wa mkoa wa Ruvuma.



WADAU WAPYA WAONGEZA NGUVU MAPAMBANO DHIDI YA VVU, MALARIA RUVUMA

Mkoa wa Ruvuma umetambulisha mashirika ya FHI360 na JHPIEGO kama wadau wapya wa maendeleo watakaotekeleza Mradi wa America First Global Health Strategy (AFGHS) katika afua za VVU na malaria mkoani humo.

Akizungumza katika kikao hicho cha utambulisho kilichofanyika leo Oktoba 27, 2026 katika Ukumbi wa Songea Club, Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Wakili Mary Gasper Makondo, ameyataka mashirika hayo kushirikiana kwa karibu na timu za afya kuimarisha utambuzi wa VVU, hususan kwa watoto, vijana, wanaume na makundi yaliyo pembezoni.

Katika hatua nyingine, amewaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri kwa kushirikiana na timu za afya na kuokoa maisha ya wananchi.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa FHI360, Dkt. Elizabeth Herman, amesema mafanikio ya mradi wa AFGHS yanategemea ushirikiano wa karibu kati ya Serikali, wadau kufanya tathmini ya huduma za kliniki za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU (CTC) ili kubaini mapungufu na kuyatatua kwa wakati.

Vilevile, kuhusu malaria, amesisitiza matumizi ya vyandarua vyenye dawa, kutokomeza mazalia ya mbu na kuhakikisha wagonjwa wanapimwa kabla ya kupewa tiba.

Kwa upande wake, mwakilishi wa Wizara ya Afya, Dkt. Emmanuel Kimario, amesema wadau wa maendeleo wana mchango mkubwa katika kuimarisha sekta ya afya nchini kupitia afua za VVU na UKIMWI, malaria, kifua kikuu (TB) na huduma nyingine muhimu za afya. Amesema ushirikiano huo unaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali za kuboresha huduma wa maendeleo, wataalamu wa afya na jamii. Ameeleza kuwa shirika hilo limejipanga kuunga mkono vipaumbele vya Serikali katika kuboresha huduma za afya na ustawi wa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.





MRADI WA UMEME KUSINI WAHITAJI KASI: SERIKALI YATOA AGIZO KWA TANESCO NA MKANDARASI



Waziri wa Nishati, Dkt. Juma Homera, ameiagiza TANESCO kuongeza usimamizi na mkandarasi wa mradi wa njia ya umeme wa kV 220 kutoka Songea–Tunduru, ili kazi ikamilike kwa wakati.
Mradi huo una sehemu mbili ambazo ni Songea–Tunduru, km 214, pamoja na Tunduru–Masasi, km 177. Ukikamilika, unalenga kuimarisha gridi ya Taifa na kuboresha upatikanaji wa umeme kwa wananchi wa Ruvuma, Lindi na Mtwara, huku ukifungua nafasi zaidi kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.
Kwa mujibu wa Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Amos Kaihula, utekelezaji wa mradi wa Songea–Masasi umefikia asilimia 56,huku sehemu ya Tunduru–Masasi ikiwa ni asilimia 34.
Mradi unatekelezwa na Kalpataru Projects International Limited ya India kwa gharama ya shilingi bilioni 150.78 kutoka Songea–Tunduru na Sh bilioni 157.69 kutoka Tunduru hadi Masasi.





UMEME WAFIKA NAKANYONYO: SH. MILIONI 82.86 KUFUNGUA FURSA MPYA ZA MAENDELEO TUNDURU

Ndoto ya wananchi wa Kitongoji cha Nakanyonyo wilayani Tunduru mkoani Ruvuma kupata umeme sasa imetimia baada ya Waziri wa Nishati, Dk. Juma Zuberi Homera, kuwasha rasmi umeme huo, hatua inayotarajiwa kuongeza shughuli za kiuchumi na huduma za kijamii katika eneo hilo.
Mradi huo umegharimu Sh. milioni 82.86, ukihusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo mdogo yenye urefu wa kilomita 1.889, ufungaji wa mashineumba yenye uwezo wa KVA 100 na kuunganisha wateja.
Takwimu za mradi zinaonesha kuwa Jimbo la Tunduru Kaskazini lina vijiji 92, vyote vikiwa vimefikiwa na miundombinu ya umeme.
Kati ya vitongoji 602, vitongoji 482 vimekwishafikiwa, huku 99 vikiwa kwenye miradi inayoendelea.
Miradi ikikamilika, vitongoji 581, sawa na asilimia 97, vitakuwa vimefikiwa na umeme.
Hata hivyo, Kata ya Nakayaya imefikia kwa asilimia 100: vijiji vyote vitano na vitongoji vyote 20 vina umeme.
Umeme huu si mwanga pekee ni mtaji wa biashara, huduma na fursa mpya za maendeleo kwa wananchi wa Tunduru.









KADERES PLC, CRDB WATAMBULISHA MRADI WA BIASHARA YA HEWA YA KABONI RUVUMA

Kampuni ya KADERES PLC kwa kushirikiana na Benki ya CRDB wametambulisha mradi wa biashara ya hewa ya kaboni mkoani Ruvuma, utakaowawezesha wakulima kuingia kwenye kilimo biashara kupitia kilimo mseto.

Uzinduzi huo umefanyika leo katika ukumbi wa Songea Club, Manispaa ya Songea, ambapo katika awamu ya kwanza, mradi unatarajiwa kusajili wakulima 60,000 kutoka halmashauri mbalimbali za mkoa huo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Mhe. Kisare Makori, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Brigedia Jenerali Ahmed Abbas, amesema mradi huo ni fursa muhimu ya biashara ya hewa ya kaboni kupitia mashamba ya chakula na biashara.

Makori ameitaka KADERES PLC kutoa elimu ya kina kwa wadau na kuandaa ziara za mafunzo ili wakulima wajifunze fursa na changamoto za mradi, kisha kujiunga kwa hiari.

Kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Katibu Tawala Msaidizi wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Yusuph Jerico Mwakatobe, amesema mkoa uko tayari kushiriki, na shughuli za kupanda miti zitakuwa sehemu ya juhudi za mkoa na taifa za kutunza mazingira.

Naye Mkurugenzi wa KADERES PLC, Leonard Kachebonaho, amesema lengo kuu ni kuwasaidia wakulima kuwekeza katika kilimo mseto kitakachowawezesha kustahimili changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Akibainisha kuwa wakulima watakaosajiliwa watanza kunufaika kupitia kilimo cha kikaboni na kupata ruzuku kwa kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa biashara ya hewa ya kaboni.

Kwa upande wake, Meneja wa mifumo ya kidigitali kilimo biashara CRDB, Allawi Mdee, amesema benki hiyo imetenga shilingi bilioni 9 kwa ajili ya kusajili wakulima wadogo. Pia, amesisitiza kuwa wakulima watakaosajiliwa hawatalazimika kutoa fedha kwa ajili ya usajili, kwani gharama zote zimeshughulikiwa na benki.





MIFUGO ISIYODHIBITIWA INAVYOCHOCHEA MIGOGORO YA WAKULIMA NA WAFUGAJI KUSINI



Mifugo inayoingia bila udhibiti imetajwa kuwa chanzo kikuu cha migogoro kati ya wakulima na wafugaji katika wilaya sita za mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma.

Hayo yamebainika katika kikao cha Kamati za Ulinzi na Usalama za mikoa hiyo kilichofanyika Nanyumbu, Mtwara, kikilenga kutafuta suluhisho la migogoro inayozidi kujitokeza hasa wakati wa kiangazi.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, aliyekuwa mwenyekiti wa kikao, alisema wilaya zilizoathirika zaidi ni Liwale na Nachingwea (Lindi), Masasi na Nanyumbu (Mtwara), pamoja na Tunduru na Namtumbo (Ruvuma).

Kwa mujibu wa Malima, migogoro hiyo imekuwa ikisababisha uharibifu wa mazao, kuvuruga amani na wakati mwingine kusababisha vifo.

Kamati hizo zimeweka mikakati ya kuhakikisha mifugo inayoingia mikoa hiyo inakuwa na vibali, vyombo vya ulinzi na usalama vinafanya kazi kwa pamoja, matukio yaliyopita yanatathminiwa na viongozi wanaopokea wafugaji kiholela wanachukuliwa hatua.

Wakuu wa mikoa hiyo wamewataka wananchi kutoa taarifa mapema kuhusu wafugaji wanaoingia bila utaratibu.

WAZIRI HOMERA ATOA AGIZO JIPYA: WANANCHI WAJENGEWE UWEZO KUTENGENEZA MAJIKO BANIFU



Lengo la Tanzania kufikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa asilimia 80 ifikapo 2034 sasa linaingia hatua mpya ya wananchi wenyewe kushiriki katika kutengeneza na kusambaza majiko banifu.

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera, ameiagiza Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuandaa utaratibu wa kuwachagua wananchi watatu kutoka kila wilaya, kuwapa mafunzo ya kutengeneza majiko banifu kwa kutumia teknolojia rahisi na malighafi zinazopatikana nchini.

Agizo hilo limetolewa Oktoba 24, 2026 wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma, wakati wa Site Trust Nishati Safi Marathon 2026.

Baada ya mafunzo, wananchi hao wanatarajiwa kuunganishwa na fursa za mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri, kwa kuzingatia vigezo na taratibu zilizowekwa.

Kwa mtazamo wa maendeleo, mpango huu unaweza kugeuza nishati safi kutoka kuwa sera pekee na kuwa fursa ya ajira, ujasiriamali na biashara za ndani.





SHILINGI MILIONI 102 ZAKUSANYWA NAMTUMBO

Zaidi ya Shilingi milioni 102 zimekusanywa kupitia Site Trust Nishati Safi Marathon 2026 kwa ajili ya kununua vifaa tiba na kuboresha huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma.

Akizungumza lOktoba 24, 2026, Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera, amesema marathon hiyo pia imelenga kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, sambamba na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2024–2034, unaolenga kufikisha matumizi ya nishati safi kwa asilimia 80 ya Watanzania ifikapo 2034.

Dkt. Homera amesema nishati safi ni muhimu katika kulinda afya za wananchi na mazingira, huku akizitaka taasisi za sekta ya nishati



kuweka mifumo itakayorahisisha wananchi kumudu gharama za teknolojia hizo.

Katika hatua hiyo, REA imetoa majiko 1,000 yanayotumia gesi, umeme na teknolojia banifu kwa ajili ya kuhamasisha matumizi yake.

Namtumbo imeunganisha afya, mazingira na nishati katika ujumbe mmoja wa matumizi ya nishati safi si anasa ni uwekezaji katika maisha ya Mtanzania.



UJENZI WA CHUO CHA UHASIBU SONGEA WAFIKIA ASILIMIA 77, RC RUVUMA ASISITIZA KASI YA UKAMILISHAJI



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, amemtaka mkandarasi anayejenga Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) Tawi la Songea kuongeza kasi ya ujenzi kwa kuongeza idadi ya wafanyakazi na kuendelea na kazi usiku na mchana ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya mradi huo unaogharimu zaidi ya Shilingi bilioni 18, Brigedia Jenerali Ahmed amesema kukamilika kwa chuo hicho kutapanua fursa za elimu ya juu kwa wananchi wa Ruvuma na maeneo jirani, sambamba na kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya mradi, Mhandisi Mshauri Juliana Wilson, amesema hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 77 ya utekelezaji, huku kazi za umaliziaji zikiendelea. Akieleza kuwa hakuna changamoto ya kifedha inayoukabili mradi huo kwa sasa, bali kinachohitajika ni kuongeza kasi ya utekelezaji ili kukamilika kwa mujibu wa ratiba.

Kwa upande wake, Meneja wa IAA Tawi la Songea, Dkt. Felista Mayunga, amesema ujenzi wa chuo hicho chenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 4,500 kwa wakati mmoja utapanua upatikanaji wa elimu ya juu katika Mkoa wa Ruvuma, na kuwataka wanafunzi pamoja na wazazi kuchangamkia fursa hiyo ili kunufaika na huduma zilizosogezwa karibu.



TANESCO YAAGIZWA KUHARAKISHA UMEME KIWANDA CHA ALUMINIUM SONGEA

Waziri wa Nishati, Dkt. Juma Homera, amelielekeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuharakisha taratibu za kuunganisha umeme katika mradi wa kiwanda cha kutengeneza aluminium unaotekelezwa eneo la Mwenge Mshindo, Manispaa ya Songea, ili kuhakikisha uwekezaji huo unaanza shughuli zake bila kuchelewa.

Ametoa maelekezo hayo leo Oktoba 23, 2026 wakati wa ziara yake katika mradi huo unaojengwa na Kampuni ya Hongwang Tanzania Holding Limited (HWTZ), akitaka mchakato wa kusaini mkataba na maandalizi mengine ya huduma ya umeme ukamilike kabla ya mwisho wa Novemba mwaka huu.

Dkt. Homera amesema uwepo wa umeme wa uhakika ni msingi muhimu wa mafanikio ya mradi huo mkubwa wa viwanda, akibainisha kuwa Serikali itaendelea kuratibu taasisi zake ili kuondoa vikwazo vinavyoweza kuchelewesha utekelezaji wa uwekezaji huo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, amesema mradi huo wenye thamani ya Shilingi trilioni 7.8 unatarajiwa kuzalisha zaidi ya ajira 5,000 mara utakapokamilika, jambo litakaloongeza shughuli za kiuchumi na kuinua kipato cha wananchi wa mkoa huo.





Amesema uwekezaji wa kiwanda hicho unaongeza hadhi ya Mkoa wa Ruvuma kama eneo muhimu la uwekezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati, sambamba na miradi mingine mikubwa ikiwemo ya Mchuchuma na Liganga inayotarajiwa kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa.

Kukamilika kwa kiwanda hicho kunatarajiwa kufungua fursa zaidi za biashara, ajira na uzalishaji wa bidhaa kwa soko la ndani na la nje, huku upatikanaji wa miundombinu muhimu ukiwa sehemu ya mafanikio ya utekelezaji wa mradi huo.

TUNDURU YAANZA KUJENGA MKAKATI MPYA WA KUMALIZA MIGOGORO YA WAKULIMA NA WAFUGAJI



Serikali imeanza kusukuma mbele mkakati wa pamoja wa kukabili migogoro kati ya wakulima na wafugaji, huku usimamizi wa ardhi, matumizi sahihi ya rasilimali na uratibu wa Serikali vikitajwa kuwa nguzo muhimu za suluhisho.

Hatua hiyo imechukuliwa , baada ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Wakili . Mary Makondo, kuongoza kikao kazi kilichowakutanisha wataalamu wa Mkoa na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

Majadiliano yalijikita katika namna ya kuimarisha maeneo ya kilimo na ufugaji, kuzuia migogoro na kuhakikisha malalamiko yanapatiwa ufumbuzi kwa wakati kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya ardhi.

Kwa mujibu wa taarifa ya kikao, lengo si kutafuta mshindi kati ya mkulima na mfugaji, bali kujenga mfumo wa matumizi ya ardhi unaowezesha makundi yote mawili kufanya shughuli zao kwa amani na kuheshimiana.

Hatua hii inaweka msisitizo kwenye kinga ya migogoro kuliko kusubiri madhara yatokee kwa kuwa amani ya jamii inaanzia kwenye usimamizi bora wa rasilimali.



KAMATI YA MAADILI RUVUMA YAAGANA NA MJUMBE, YASISITIZWA UADILIFU KAZINI

Kamati ya Maadili ya Maafisa wa Mahakama ngazi ya Mkoa wa Ruvuma imefanya kikao chake cha robo ya kwanza, ambapo pamoja na mambo mengine yaliyojadiliwa, Kamati ilitumia fursa hiyo kumuaga mjumbe wa kamati hiyo, Mhe. Asha Waziri, Hakimu Mkazi Mfawidhi, Mahakama ya Hakimu Mkazi, ambaye kwa sasa ameteuliwa kuwa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Masjala Ndogo ya Dodoma.

Kikao hicho kiliongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, ambaye amempongeza Mhe. Asha Waziri kwa utumishi wake ndani ya Mkoa na kumtakia mafanikio katika majukumu yake mapya.

Katika kikao hicho, Brig. Gen. Ahmed Abbas baada ya kuarifiwa kutokuwepo na Malalamiko dhidi ya Maafisa wa Mahakama katika kipindi cha robo ya kwanza 2026/2027, ameonesha kuridhishwa na utendaji wa Maafisa hao, huku akibainisha kuwa Mhimili wa Mahakama umeendelea kuimarisha misingi ya Maadili na uwajibakaji.





Hata hivyo, amewataka wajumbe wa kamati ambao miongoni mwao ni Maafisa wa Mahakama kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, uadilifu na kuzingatia maadili ya kazi, huku akisisitiza umuhimu wa kujipima mara kwa mara katika utendaji wao ili kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

RUVUMA YALENGA TANI 30,000 ZA KAHAWA, WAKULIMA WAPEWA MICHE 450,000



Msimu huu mkoa wa Ruvuma Unalenga kuvuka rekodi ya msimu uliopita kwa kuzalisha tani 30,000 za kahawa, kutoka tani 26,000 zilizozalishwa msimu uliopita sawa na ongezeko la takribani asilimia 15.4.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Kahawa Duniani, Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Mhe. Peres Magiri, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, amesema Serikali inaweka nguvu kwenye kuongeza tija, ubora na thamani ya kahawa ili kuongeza kipato cha wakulima.

Miongoni mwa mikakati ni usajili wa wakulima, kuajiri na kutoa mafunzo kwa vijana zaidi ya 120, pamoja na uzalishaji na usambazaji wa miche bora. Serikali inatarajia kutoa miche 450,000 kwa wakulima.

Afisa Ushirika Wilaya ya Nyasa, Menas Ndomba, amesema maadhimisho hayo ni fursa ya kuwaunganisha wadau na kuonesha thamani ya kahawa katika kuinua kipato cha wakulima.

Naye Mrajis Msaidizi wa Ushirika Mkoa wa Ruvuma, Venance Msafiri, amezitaka halmashauri kuanzisha mashamba ya miche yatakayotumika kama mashamba darasa, akitolea mfano Halmashauri ya Mbinga.

Lengo ni tani 30,000; lakini ushindi wa kweli utapimwa kwa ubora wa kahawa na ongezeko la kipato cha mkulima.



WANANCHI WAHIMIZWA KUTUMIA CHATBOT KUPATA HUDUMA ZA TANESCO

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Ruvuma limewahamasisha wananchi kutumia mfumo wa Chatbot unaopatikana kupitia WhatsApp, likisema huduma hiyo inarahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali za umeme bila kulazimika kufika ofisini.

Akizungumza na wadau katika Wiki ya Huduma kwa Wateja, Afisa Mahusiano wa TANESCO Mkoa wa Ruvuma, Allan Njiro, amesema Chatbot ni miongoni mwa njia zinazowawezesha wateja kupata huduma kwa haraka, ikiwemo token za umeme, taarifa za huduma na maombi ya kuunganishiwa umeme.

Njiro amesema TANESCO imeingia makubaliano na Benki ya CRDB kuwezesha wananchi kulipia huduma ya TPG kwa urahisi, pamoja na kuandaa utaratibu wa mikopo ya gharama za kuunganishiwa umeme kwa wananchi wa vijijini.



Kwa upande wake, Mhandisi Boniface Malibe amesema TANESCO Mkoa wa Ruvuma imejipanga kukabiliana na athari za mvua kubwa kwa kukagua miundombinu, kubadilisha nguzo chakavu, kukata miti inayohatarisha njia za umeme na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu usalama wa umeme.

Malibe amewataka wananchi kulinda miundombinu ya umeme kwa kutoa taarifa za vitendo vya uharibifu, wizi au waya zinazoanguka wakati wa mvua, akisisitiza kuwa usalama wa miundombinu hiyo ni jukumu la kila mwananchi.



TANESCO RUVUMA YAREJESHA KIVUKO MISUFINI – MATARAWE



Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Ruvuma limetumia Wiki ya Huduma kwa Wateja kurejesha usalama wa kivuko cha Mto Matarawe kinachounganisha Kata za Misufini na Matarawe, Manispaa ya Songea, baada ya kivuko cha awali kuwa hatarishi kwa watumiaji.

Afisa Usalama wa TANESCO Ruvuma, Said Sombwe, amesema hatua hiyo ni sehemu ya kujali jamii, licha ya jukumu kuu la shirika hilo kuwa ni kusambaza umeme.

Amesisitiza kuwa kivuko hicho ni kiungo muhimu kwa wananchi wakiwemo wanafunzi, wazee wanaovuka kila siku, hivyo usalama wao ni kipaumbele.

Naye Diwani wa Misufini, Mariam Nchimbi, amesema wananchi walikuwa wakikabiliwa na changamoto kubwa kutokana na hali ya kivuko, hususan wanafunzi waliokuwa wakielekea shuleni.

Kwa upande wake, Diwani wa Matarawe, Joel Makuburi, amebainisha kuwa awali baadhi ya watumiaji walipata ajali wakati wa kuvuka, hivyo hatua ya TANESCO imekuwa suluhisho la muda mrefu.



VIONGOZI WATAKIWA KUTEKELEZA MAJUKUMU KWA KUZINGATIA MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, amewaagiza wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya pamoja na wakurugenzi wa halmashauri mkoani humo kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na maadili ya utumishi wa umma.

Akizungumza katika kikao na viongozi hao kilichofanyika Ikulu Ndogo mjini Songea, amesema viongozi hao wanapaswa kuwa mstari wa mbele kutatua changamoto za wananchi na kuhakikisha huduma za serikali zinawafikia kwa ufanisi.

Pia amewataka kuongeza juhudi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuhakikisha fedha zinazokusanywa zinatumika ipasavyo kutekeleza miradi ya maendeleo yenye manufaa kwa wananchi.

Vilevile, amesisitiza umuhimu wa kudumisha amani na usalama katika wilaya na halmashauri zote za mkoa huo ili kuweka mazingira bora ya maendeleo na uwekezaji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Beatrice Mwinuka, amesema serikali imeendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hivyo ataongeza usimamizi wa miradi hiyo na kuhakikisha ukusanyaji wa mapato unafanyika kwa ufanisi ili kuboresha huduma kwa wananchi.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Madaba, Samson Abas Sanga, ameahidi kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo na kuhakikisha thamani ya fedha za serikali inaonekana kupitia utoaji wa huduma bora kwa wananchi.



ARDHI YA UWEKEZAJI LAZIMA IZALISHE AJIRA NA KUWANUFAISHA WANANCHI

Serikali imeweka wazi kuwa ardhi inayotolewa kwa uwekezaji si nafasi ya kukalia bila kutekeleza ahadi: Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kaspar Mmuya, amemtaka mwekezaji wa SOAGRO, Dkt. Joseph Kizito, kutekeleza kikamilifu mpango wa uwekezaji uliowasilishwa.

Mmuya ametoa agizo hilo baada ya kukagua Shamba la Mifugo Lilahi, Muhukuru wilayani Songea mkoani Ruvuma na kumkabidhi mwekezaji hati ya umiliki.

Takwimu zinaonesha ukubwa wa mpango huo: Serikali inalenga kutenga hekta milioni 6 za mifugo ndani ya miaka mitano, huku zaidi ya hekta milioni 3.4 zikiwa tayari zimetambuliwa na kupimwa hadi Juni 2026. Serikali pia imetenga Sh bilioni 38 kwa upimaji na upangaji wa matumizi ya ardhi katika vijiji 1,460.

Kwa SOAGRO, lengo ni kufikisha ng'ombe 2,000, kondoo 10,000 na mbuzi 4,000, huku ajira zikilenga kufikia 279 za kudumu na zaidi ya ajira 400 za muda ifikapo 2031.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas, amesema uwekezaji huo unaweza kusaidia kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji kupitia malisho, maji na majosho.

Kwa upande wake Mwekezaji Dkt. Joseph Kizito amesema SOAGRO tayari imejenga maboma, nyumba, barabara za kilomita 32 na kusambaza maji.





RC RUVUMA AWATAKA WATUMISHI WA UMMA KUWA WAADILIFU NA WAAMINIFU



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, amewataka watumishi wa umma kuwa waadilifu na waaminifu katika kutekeleza majukumu yao ya kuwahudumia wananchi, huku akiwataka kumtanguliza Mungu katika kila jambo.

Akizungumza katika hafla ya kumuaga Brigedia Jenerali John Ndunguru, aliyekuwa Kamati ya Usalama ya Mkoa wa Ruvuma na anayehamia Mkoa wa Tabora. Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed amesema kila mtu amewekewa nafasi yake na Mungu, hivyo hakuna binadamu anayepaswa kuingilia au kuharibu nafasi ya mwingine.

Amesema watumishi wa umma wanapaswa kushirikiana na kusaidiana katika utekelezaji wa majukumu yao, badala ya kufanya vitendo vinavyoweza kuhatarisha au kuharibu nafasi za wenzao.

Kwa upande wake, Brigedia Jenerali John Ndunguru amewataka viongozi kuwa waadilifu na waaminifu kwa wananchi wanaowaongoza, akisisitiza kuwa uongozi unahitaji kujenga mazingira ya kuleta tija na maendeleo katika jamii.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Wakili Mary Makondo, amesema uongozi ni kujali na kugusa maisha ya jamii anayoiongoza. Ameongeza kuwa anamshukuru Brigedia Jenerali



John Ndunguru kwa kuwa kiongozi aliyejali na kugusa maisha ya wananchi wa Ruvuma wakati wa uongozi wake

CCM RUVUMA YAHIMIZWA KUJENGA UCHUMI, KUFANYA SIASA SAFI



Wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Ruvuma wametakiwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi sambamba na kufanya siasa safi ili kuimarisha maendeleo ya chama na ustawi wa mwananchi mmoja mmoja.

Wito huo umetolewa na Mlezi wa CCM Mkoa wa Ruvuma, Hamad Chande, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, wakati wa uzinduzi wa vibanda 20 vya biashara vyenye thamani ya shilingi milioni 100 katika Kata ya Mshangano, Manispaa ya Songea, Novemba 3, 2026.

Chande amesema siasa na uchumi ni nguzo zinazotegemeana, akisisitiza kuwa uchumi imara ndio msingi wa uendeshaji wa shughuli za kisiasa na maendeleo ya chama.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma, Oddo Mwisho, amesema chama kinaendelea kutekeleza maelekezo ya Mwenyekiti wa CCM Taifa na Rais wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuanzisha na kuendeleza miradi ya kiuchumi katika maeneo ya chama ili kuongeza mapato na kuzalisha ajira kwa vijana.

Kwa upande wake, Katibu wa CCM Mkoa wa Ruvuma, Mohamed Aly, amesema eneo la Mshangano lina jumla ya vibanda 90 vya biashara, ambapo vibanda 20 vimefunguliwa rasmi kwa matumizi. Ameongeza kuwa chama kina mpango wa kujenga jengo la ghorofa katika eneo hilo litakalotumika kama ofisi ya CCM wilaya ya Songea

MLEZI WA CCM RUVUMA ASISITIZA UMOJA NA MSHIKAMANO

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mlezi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Ruvuma, (MCC), Hamad Hassan Chande amewataka viongozi na wanachama wa chama hicho kuendeleza umoja, mshikamano na ushirikiano katika kukijenga na kukiimarisha chama ili kuendelea kuwapatia maendeleo wananchi.

Chande amesema hayo leo Novemba 2, 2026, mara baada ya kuwasili na kuzungunza na viongozi na wanachama wa chama hicho licha ya kupongeza uongozi wa Mkoa huo kwa jitihada kubwa za kuendelea kukijenga chama kwa lengo la kulipatia Taifa maendeleo.

"Nimekuja kuungana nanyi ndugu zangu kwa lengo moja tu, nimekuja kuimarisha Chama Cha Mapinduzi, ujenzi wa Chama Cha Mapinduzi, kipo imara, kipo fiti, lakini lazima tukae pamoja ili tujenge kwa pamoja" Chande

Katika hatua nyingine, Chande amemshukuru Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Taifa, kwa kumuamini kuwa mjumbe na kuwatumikia wanachama na wananchi wa Mkoa huo, huku aliweka dhamira ya dhati katika kuimarisha chama kikamilifu kwa kushirikiana na uongozi na wanachama wa Mkoa huo.







SONGEA DC YAWEKA MKAKATI WA DHARURA SOKO LA PERAMIHO KABLA YA MVUA KUBWA



Soko la Peramiho lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma limeanza kujiandaa kukabiliana na athari za mvua za El Niño, huku wafanyabiashara wakitakiwa kubeba jukumu kubwa katika kudhibiti uchafu, maji kutuama na kuziba kwa mifereji.

Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti wa Taka na Usafi wa Mazingira wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Makisio Chengula, amesema kila mfanyabiashara anatakiwa kusafisha eneo lake la biashara kila siku.

Chengula pia ametaka kuwepo kwa usafi wa pamoja kila Jumamosi ya mwisho wa wiki, hatua inayolenga kuweka soko katika mazingira salama kwa wafanyabiashara na wananchi.

Kwa mujibu wa Halmashauri, hatua hiyo inalenga kupunguza hatari zinazoweza kuchochewa na mvua, ikiwemo maji kutuama, kuziba kwa mifereji na kuenea kwa magonjwa yanayohusishwa na uchafu wa mazingira.

Wafanyabiashara wa Soko la Peramiho wameunga mkono mpango huo na kuahidi kushirikiana katika utekelezaji wa maazimio.



CHAKULA CHA ASILI SILAHA DHIDI YA MAGONJWA

Sahani ya chakula inaweza kuwa sehemu ya kinga ya afya ya familia. Huo ndio ujumbe uliotawala kwenye kilele cha Siku ya Lishe Kitaifa katika Kituo cha Afya Mpandangindo Halmashauri ya wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.

Diwani wa Viti Maalum wa Kata ya Mpandangindo, Mhe. Elizabeth Mapunda, amewataka wananchi kula zaidi vyakula vya asili vinavyopatikana katika mazingira yao na kuzingatia mlo kamili, akisisitiza kuwa lishe bora ni msingi wa afya na inaweza kusaidia kupunguza vihatarishi vya magonjwa yasiyoambukiza.

“Imarisha afya , Kula Kiasili, Punguza Sukari, Chumvi na Mafuta” ndiyo kaulimbiu ya maadhimisho hayo.

Kwa upande wake, Mratibu wa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea,Joyce Sipira, amesisitiza ulaji wa makundi yote ya chakula ili familia zipate virutubishi muhimu.

Maadhimisho hayo pia yalihusisha tathmini ya hali ya lishe kwa watoto na watu wazima pamoja na upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza.



NMB YAPELEKA MADAWATI, VITI NA KOMPYUTA TUNDURU: SHILINGI MILIONI 16.59 ZATUMIKA KUBORESHA ELIMU



Benki ya NMB imewekeza Sh milioni 16.59 kuboresha mazingira ya kujifunzia katika shule za Tunduru, kupitia utoaji wa samani na vifaa vya TEHAMA.

Katika makabidhiano yaliyofanyika Shule ya Msingi Mlingoti, NMB imekabidhi madawati 100 kwa Shule za Msingi Muungano na Mchoteka, pamoja na meza na viti 50 kwa Mlingoti.

Kwa upande wa TEHAMA, shule tatu za sekondari zimepatiwa kompyuta za mezani 12—Tunduru Sekondari, Kungu Sekondari na Masonya Sekondari, kila moja ikipokea kompyuta nne.

Meneja wa Kanda wa NMB, Bi. Olipa Hebel, amesema fedha hizo zimetumika kugharamia vifaa vilivyotolewa.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Denis Masanja, Katibu Tawala wa Wilaya, Milongo Sanga, ameipongeza NMB na kuitaka kupanua zaidi uwekezaji wa kijamii katika sekta nyingine za maendeleo.

Kwa mtazamo mpana, mchango huo unaweka mkazo kwenye mazingira bora ya kujifunzia, upatikanaji wa TEHAMA na ushirikiano kati ya sekta binafsi na Serikali.

ONE HEALTH SOCIETY KUTEKELEZA MRADI WA AFYA YA WANAWAKE RUVUMA

Taasisi ya One Health Society kwa kushirikiana na wadau wake, SarataniAI na Street Afya, imetambulisha programu maalumu ya kuimarisha afya ya wanawake mkoani Ruvuma kupitia mradi utakaotekelezwa katika Wilaya ya Tunduru kuanzia Novemba 2026.

Programu hiyo ilitambulishwa wakati wa ziara ya heshima ya taasisi hiyo katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, ambapo ujumbe huo ulikutana na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa, Bw. Joel Mbewa, pamoja na Mganga Mkuu wa Mkoa, Dkt. Louis Chomboko.

Mradi huo wa Transforming Public Health for Community Resilience unafadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nje, Jumuiya ya Madola na Maendeleo ya Uingereza (UK FCDO) kupitia Mfuko wa Programu za Wahitimu wa Chevening (CAPF), ukiwa na lengo la kuboresha huduma za afya ya wanawake na kuchochea uwezeshaji wa kiuchumi katika jamii.

Kupitia utekelezaji wake, watoa huduma za afya walio mstari wa mbele watapatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo, huku jamii ikifikiwa na elimu na uhamasishaji kuhusu masuala mbalimbali ya afya.

Vilevile, wanawake watapatiwa huduma za uchunguzi jumuishi wa Kichocho cha Via vya Uzazi (FGS), saratani ya mlango wa kizazi na VVU, sambamba na mafunzo ya elimu ya fedha yatakayowawezesha kujikwamua kiuchumi.

Akizungumza katika kikao hicho, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Bw. Joel Mbewa, ameipongeza One Health Society na washirika wake kwa kuileta programu hiyo mkoani humo, akisisitiza kuwa ushirikiano wa wadau mbalimbali utasaidia kufanikisha malengo yaliyokusudiwa na kuwanufaisha wananchi.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Mkoa, Dkt. Louis Chomboko, ameeleza umuhimu wa ushirikiano kati ya Serikali na wadau wa maendeleo katika kuimarisha huduma za afya, hususan kwa wanawake ambao ni mhimili muhimu wa maendeleo ya familia na jamii.

Uongozi wa One Health Society umeeleza kuwa unatarajia kushirikiana kwa karibu na viongozi wa mkoa, wilaya na wadau wengine ili kuhakikisha utekelezaji wa programu hiyo unakuwa na matokeo chanya katika kuboresha afya na ustawi wa wanawake pamoja na jamii kwa ujumla







ZAIDI YA BILIONI 3.17 ZAGEUKA HUDUMA HOSPITALI YA SONGEA: WANANCHI WAPATA MATIBABU KARIBU NAO



Uwekezaji wa zaidi ya Shilingi bilioni 3.17 katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea, iliyopo Mpitimbi, umeongeza uwezo wa wananchi kupata huduma muhimu za afya bila kusafiri umbali mrefu.

Hospitali hiyo sasa inatoa huduma za X-ray, upasuaji, macho, meno na uzazi, ikiwemo upasuaji wa kina mama.

Mganga Mfawidhi, Dkt. Sakina Komesha, amesema vifaa na huduma hizo zimewezesha wagonjwa kupata matibabu karibu na maeneo yao.

Mganga Mkuu wa Halmashauri, Dkt. Zaituni Hamza, amesema uwekezaji katika miundombinu, vifaa tiba na wataalamu umeimarisha uwezo wa hospitali kuhudumia wagonjwa, wakiwemo watoto.

Kwa wananchi, mabadiliko hayo yanamaanisha kupungua kwa gharama za usafiri, usumbufu na ucheleweshaji wa matibabu.

Mkazi wa Nambendo, Fatuma Umbala, amesimulia namna alivyopokelewa na kuhudumiwa haraka alipomfikisha mgonjwa kwa ajili ya kujifungua.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Elizabeth Gumbo, amesema uwekezaji huo umeongeza fursa ya wananchi kupata huduma karibu na makazi yao.



MTO RUVUMA: HAZINA YA TANZANIA INAYOWEZA KUGEUKA CHAPA KUBWA YA UTALII, UCHUMI NA HISTORIA AFRIKA

Maji yanayoanzia katika milima ya Matogoro mjini Songea yana simulizi kubwa kuliko unavyoweza kufikiria.Mto Ruvuma, rasilimali inayounganisha Tanzania na Msumbiji, huku ikibeba fursa za mabilioni ya maendeleo kupitia kilimo, uvuvi, nishati, biashara na utalii.

Kwa mujibu wa taarifa za Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini, mto huo una urefu wa takribani kilomita 800, huku karibu kilomita 650 zikitumika kama mpaka wa Tanzania na Msumbiji.

Utafiti wa ICLEI (Local Governments for Sustainability) wa mwaka 2018 unakadiria kuwa takribani watu milioni 2.4 wanategemea rasilimali za bonde hilo.

Katika kijiji chaLipokela wilayani Songea, shamba la AVIV Tanzania lina zaidi ya hekta 2,000, zaidi ya hekta 1,000 zikiwa zimepandwa kahawa na mto Ruvuma unatumika katika kilimo cha umwagiliaji.

Meneja Msaidizi, Muthana Maruvanda, anasema takribani asilimia 60 ya kahawa inayozalishwa huuzwa nje ya nchi.

Mto Ruvuma katika daraja la Umoja, Mtambaswala, linaongeza thamani ya kiuchumi na kijamii kwa kuunganisha Tanzania na Msumbiji. Afisa Mahusiano wa Kituo cha Uhamiaji Mtambaswala, Mwamba Lihami, anataja pia fursa za elimu na utalii katika makutano ya mito Ruvuma na Rujenda.

Mkazi wa Wenje, Tunduru, Rashid Juma, anasema mto huo ni tegemeo la wananchi kupitia uvuvi na kipato.

Changamoto sasa ni kugeuza utajiri huu kuwa maendeleo endelevu. Mto Ruvuma si mpaka unaotenganisha mataifa; ni hazina inayoweza kuyaunganisha ustawi wa vizazi vijavyo.





SIRI YA HANDAKI CHINI YA ARDHI SONGEA: NDANI YA MAKUMBUSHO YA KAWAWA KUNA HISTORIA AMBAYO WATANZANIA WENGI HAWAIFAHAMU!

Nyuma ya kuta za jengo moja lililopo Bombambili mjini Songea mkoani Ruvuma kuna historia inayoweza kubadilisha namna unavyoitazama safari ya ukombozi wa Tanzania.

Handaki la siri, mavazi, medali na picha za kihistoria ni miongoni mwa hazina zinazohifadhiwa katika Makumbusho ya Kumbukumbu ya Dkt. Rashid Mfaume Kawawa. Makumbusho hayo yalifunguliwa rasmi Februari 27, 2017, tarehe ya kuzaliwa kwa Kawawa, yakilenga kuhifadhi historia ya mmoja wa viongozi muhimu katika harakati za ukombozi wa Tanganyika.

Ndani yake, wageni wanaweza kuona mavazi aliyovaa, samani alizotumia, vitabu, medali na picha zinazoibua sehemu mbalimbali za maisha yake.

Hata hivyo, handaki la siri ndilo mojawapo ya vivutio vinavyovuta hisia zaidi, likikumbusha mazingira ya maficho na mapambano ya kipindi cha ukombozi.

Mhifadhi Kiongozi wa makumbusho hayo, James Mfikwa, anasema makumbusho hayo si kumbukumbu ya mtu mmoja pekee, bali ni hazina ya historia ya Tanzania na Afrika.

Jambo jingine la kuvutia ni historia ya Kawawa katika filamu za Kiswahili, akihusishwa na kazi za miaka ya 1950, zikiwemo filamu za Muhogo Mchungu (1951), Meli Inakwenda (1952) na Juma Matatani (1954).





SIRI YA HOSPITALI YA ST.ANNES LIULI ILIANZA KWA KUJENGWA KWA MATETE MWAKA 1902



kuhifadhiwa kwa vizazi vijavyo.

Kabla ya historia kuandikwa kwenye vitabu, Hospitali ya Mtakatifu Anna (Saint Anne's) iliyopo Liuli wilayani Nyasa mkoani Ruvuma ilikuwa sehemu ya simulizi ya vita, majeraha na mapambano dhidi ya ukoloni wa Kijerumani.

Ilianzishwa mwaka 1902, hospitali hii inahusishwa na Vita ya Majima-ji vya mwaka 1905–1907. Mwaka 1906, ilitumika kuwahudumia majeruhi wa vita hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa za kihistoria , zaidi ya wapiganaji 3,000 walipata huduma katika hospitali hiyo.

Takwimu hiyo inaipa hospitali hii nafasi muhimu katika historia ya huduma za afya na kumbukumbu za mapambano dhidi ya ukoloni.

Hata hivyo, historia yake haiku-wa rahisi. Gift Mtega, Katibu na Msimamizi Mkuu wa hospitali hiyo, anasema kituo hicho kilianza nyuma ya jiwe la Pomonda, lakini kupanda kwa maji ya Ziwa Nyasa kulilazimisha kuhamishwa.

Anasema majengo ya awali yaliyo-jengwa kwa matete yaliharibiwa na mchwa hali iliyosababisha hospi-tali kuhamishiwa eneo la juu zaidi mwaka 1928.

Leo, simulizi ya Saint Anne's Liuli inakumbusha kuwa hospitali zin-aweza kuwa zaidi ya vituo vya tiba: ni hazina za historia zinazostahili

JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA
Kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma
S.L.P 74 SONGEA
57180 RUVUMMA
SIMU Nambari; 025-22602256/2602238
FAX No.2602144
E-MAIL ras.ruvumatamisemi@go.tz
TOVUTI:www.ruvuma.go.tz
INSTAGRAM:rs Ruvuma
FACEBOOK:rs Ruvuma
YOUTUBE: rs Ruvuma